REPUBLIC OF KENYA

COUNTY ASSEMBLY OF LAIKIPIA

THE HANSARD

Tuesday, 7th June, 2022

The House met at the Assembly Chambers at 2.47 p.m.

[Deputy Speaker (Hon. Daniel Nyausi) in the Chair]

PRAYERS

COMMUNICATION FROM THE CHAIR

APOLOGIES FOR LATENESS

Deputy Speaker: Hon. Members, I would like to apologize for coming late. I was unable to be here on time because of the situation we are in but that should not be an excuse. I'm sorry and I apologize. Next time will try to be on time. Thanks.

PAPERS LAID

QUARTERLY REPORT AND FINANCIAL STATEMENTS FOR THE DEPARTMENT OF AGRICULTURE, LIVESTOCK AND FISHERIES

Hon. Stephen Ndiritu: Thank you Mr. Speaker. On behalf of the Chairperson for Agriculture, Hon. Kanyutu I would like to lay a quarterly report and financial statement for period ended 31st March, 2021. Thank you.

(Hon. Stephen Ndiritu laid the Paper on the Table)

QUARTERLY REPORT AND FINANCIAL STATEMENTS FOR THE DEPARTMENT OF FINANCE, PLANNING AND COUNTY DEVELOPMENT

Hon. Joseph Suge: Hon. Speaker, on behalf of the Chairperson for the Finance Committee, I would like to lay a report by the Committee of Finance and County Planning on County Government of Laikipia (Executive) third quarter report and financial statements for the period ended 31st March, 2021 for the Department of Finance, Planning and County development. Thank you.

(Hon. Joseph Suge laid the Paper on the Table)

QUARTERLY REPORT AND FINANCIAL STATEMENTS FOR THE DEPARTMENT OF ROADS, LANDS AND ENERGY

Hon. Daniel Mugweru: Thank you Hon. Speaker. I beg to lay a paper on quarterly report and financial statements for the period ended 31st March, 2021 for the Department of Roads, Lands and Energy by the Sectoral committee on Transport and Public works dated 6th June 2022. Thank you.

(Hon. Daniel Mugweru laid the Paper on the Table)

NOTICES OF MOTION

QUARTERLY REPORT AND FINANCIAL STATEMENTS FOR THE DEPARTMENT OF AGRICULTURE, LIVESTOCK AND FISHERIES

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. Stephen Ndiritu: Thank you Mr. Speaker. On behalf of the Chairperson for Agriculture, Hon. Kanyutu representing the people of Marmanet, I beg to give notice of this motion;

> THAT, this House adopts the quarterly report and financial statement for period ended 31st March, 2021 for Department of Agriculture, Livestock and Fisheries by the Sectoral committee on Agriculture, Environment and Natural resources dated 25th May, 2022. Thank you.

QUARTERLY REPORT AND FINANCIAL STATEMENTS FOR THE DEPARTMENT OF FINANCE, PLANNING AND COUNTY DEVELOPMENT

Hon. Joseph Suge: Hon. Speaker, on behalf of Hon. Mary Samken Chair, Finance and County Planning I beg to give notice of the following motion;

> THAT, this House adopts the quarterly report and financial statements for the period ended 31st March, 2021 for Department of Finance, Planning and County Development by Sectoral Committee on Finance and Planning. Thank you.

QUARTERLY REPORT AND FINANCIAL STATEMENTS FOR THE DEPARTMENT OF ROADS, PUBLIC WORKS, LANDS AND ENERGY

Hon. Daniel Mugweru: Thank you Hon. Speaker. I beg to give notice of the following motion;

> THAT this Assembly adopts the quarterly report and financial statement for period ended 31st March, 2021 for the Department of Roads, Public Works, Lands and Energy by the Sectoral committee on Transport and Public works dated 6th June 2022. Thank you.

MOTION

QUARTERLY REPORT AND FINANCIAL STATEMENTS FOR THE DEPARTMENT OF ROADS, PUBLIC WORKS, LANDS AND ENERGY

Hon. Daniel Mugweru: Thank you, Hon. Speaker. I beg to move the following motion;

> THAT this Assembly adopts the quarterly report and financial statement for period ended 31st March, 2021 for the Department of Roads, Public Works, Lands and Energy by the Sectoral committee on Transport and Public works dated 6th June 2022.

Hon. Speaker, the department of roads and Public works is composed of five Members.

1. Hon. Daniel Mugweru - Chairperson
2. Hon. Stephen Nderitu - Vice Chairperson
3. Hon. Wilson Wakahiu - Member
4. Hon. Mary Samken - Member
5. Hon. Catherine Nyawira - Member

Hon. Speaker, each Member has a report and I can only move directly to the observations in that quarter. As usual in this County, we noted there was a pending bill of Kshs. 275,083,723. The biggest percentage in that is the civil works/the road works that had Kshs. 267,296,454. Hon. Speaker, this is a reflection of how our county is because the people of Laikipia are enjoying good roads and service. The provider of those services has not been paid.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

When Kshs. 275,083,723 is not circulating, this means there are thousands of people suffering. If this money was paid to the contractors who provided services, maybe the money would be circulating. It also means there is somebody somewhere who is sited sick in mind because he acquired a loan from a bank and has not acquired payment from this County.

Mr. Speaker, it is so important, and that is what the Committee observed; that these big pending bills, if we do not stick within the actual budget then we will be finding ourselves in these problems. The committee recommended that the department should always ensure that the projects that are committed are within the actual budget allocation because we need to prevent these pending bills.

Having said that, it is also important to note that the budget itself, the Kshs.275 million, being in the Department of Roads and still Laikipians are suffering, they are still claiming that there are roads which are not passable. It means that when we are making our budget, we should even increase the allocation for this department. I call upon Hon. Members to support this report and as I do so, I also wish to thank you, Hon. Speaker, because of apologizing for coming late; it is not normal and we have taken it politely. It is good to apologize for coming late, because those who apologize are always forgiven and life is very safe for them. We are really grateful about that.

I call upon Hon. Stephen Ndiritu who is a Member of this House representing the people of Thingithu in this Second Assembly and who we believe will be representing them in the Third Assembly. Without fear, I can really confirm that he will be representing them in this House. I am calling upon him to second this motion. Thank you.

Deputy Speaker: The incoming Member of Thingithu?

Hon. Stephen Ndiritu: Asante sana, Mheshimiwa Spika. Wajua Mswahili husema kwamba lisemwalo lipo, na kama halipo laja. Nataka kumshukuru Nabii Mugweru kwa hayo maneno ya ujasiri na hekima na ningeomba iwe hivyo na iwe amina.

Mheshimiwa Spika, nataka kusimama kuunga mkono ripoti hii kutoka kwa Idara ya Miundo Msingi. Kazi ya idara hii sanasana ni kuhakikisha kuwa wananchi wa Laikipia wanapata huduma kama vile barabara, nyumba, na kuhakikisha kuwa watu wanaishi vizuri katika Kaunti ya Laikipia na barabara pamoja na nyumba zote ziko sawa. Idara hii inahusika pia na mambo mengi ya ujenzi kwenye idara tofauti.

Sisi kama kamati tumeweza kuwa na hii ripoti na kuikagua na kuona maoni ambayo kamati imetoa. Kamati imeweza kuona kuwa kuna shida katika hii idara, ikizingatiwa kwamba hii ni ripoti ya robo ya mwaka iliyoisha tarehe 31 mwezi wa tatu. Pesa zilizo hapa ambazo ni deni, hata kama tungeweza kusema hiyo idara inaweza kulipa hizo pesa haraka, utaona kwamba hizo ni pesa nyingi sana. Hizo pesa ni zile ambazo makandarasi waliofanya kazi hawajalipwa. Pengine kuna mfanyakazi wa mkono wa Laikipia aliyefanya kazi lakini hakulipwa.

Tukiwa tunaona mambo kama haya, yanatutia wasiwasi na tungetaka Wajumbe, kwa sababu wameweza kuyaangalia, wajue hivyo ndivyo ilikuwa na hayo ndiyo mambo yanayoendelea katika hiyo idara. Kama sisi tungeweza kuhakikisha ya kwamba hao watu tumewachunguza vizuri na tuhakikishe ya kwamba kazi inafanyika vile inavyostahili tungeweza kuwaokoa wananchi wanaoteseka bila barabara na makandarasi ambao sasa hivi hawana kazi kwa sababu sisi katika Kaunti yetu ya Laikipia tuliwanyang'anya makandarasi wa hapa kazi na kuwapa mabwanyenye kutoka Nairobi.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Nasema hivyo kwa sababu wakati tunaona Kaunti ya Laikipia haina makandarasi ambao wanatengeneza barabara hapa, na wanaotengeneza barabara hapa ni kampuni ya Rentco, ambayo...

Deputy Speaker: Order! Hon. Ndiritu. Hon. Member representing the people of...

Hon. Stephen Ndiritu: Thank you for forgetting.

Deputy Speaker: Hon. John Mutahi, the Member is seconding. So please allow him to second and from there the other debates will follow, thank you.

Hon. Stephen Ndiritu: Asante, Bwana Spika kwa kunilinda dhidi ya Mheshimiwa Mutahi. Ningependa kuendelea kwamba tunaona zile barabara zinazojengwa hapa kupitia ukodishaji, ni kampuni ya Rentco. Ukiangalia wenye hio kampuni, ni mabwanyenye, ni Wahindi. Nikiangalia Kaunti yetu ya Laikipia sioni kama kuna Mhindi, na kama yuko ni yule tu anayeuza unga hapa, ambaye ni Galwale na wengine ambao hatuwajui.

Kwa hivyo ningetaka, katika Kaunti yetu ya Laikipia, hata kama tutakuwa na mpango wa ukodishaji, ni vizuri tuwainue makandarasi walio hapa na ambao ni watu wa Laikipia. Maana ya Ugatuzi ilikuwa ni kwamba pesa ambazo zitakuja hapa ziwasaidie wananchi wa Laikipia na kusaidia makandarasi walio hapa. Walio Nairobi wasaidiwe na Kaunti hiyo nyingine, walio Mombasa wasaidiwe na walio Mombasa. Hii serikali ya Kaunti ya Laikipia imekuwa ya mabwanyenye na watu ambao pengine hawajali watu wa Laikipia, ila tunangoja tarehe tisa ambapo hii serikali ya mabwanyenye inaenda nyumbani na serikali ya *Mahustler* kuchukua usukani.

Kwa hivyo, nataka kuunga mkono ripoti hii na kuwaomba wengine wote walio na moyo mkunjufu, moyo wa kuweza kushikilia watu wa Laikipia, tupitishe hii ripoti na kuungana na mwenyekiti ambaye ametuambia ukweli wa mambo jinsi ambavyo Kaunti ya Laikipia imekaa na deni ambazo ziko. Asante sana, naunga mkono na kuafiki mswada.

(Question proposed)

Hon. Mutahi Muritu: Mheshimiwa Spika, nimekuta mtaalamu kutoka Thingithu akisema kwamba kampuni zilizopewa kandarasi ni mabwanyenye na ana uhakika zaidi kwamba sijui tarehe tisa wataleta hiyo serikali ya *Mahustler*. Mimi sijui kama kuna kitu kinaitwa *Mahustler*. Cha muhimu ni kusema kwamba yeye alikuwa kwenye hili Bunge tulipopitisha huo mswada ambao uliidhinisha Rentco East Africa iwe mtoa kandarasi ndani ya hili Bunge.

Kwa hivyo mtu anaposema hii ni serikali ya maskini na matajiri, ni vizuri wakati mwingine tuwe tunaogopa mungu. Yeye amekuwa kwenye hiyo serikali, amejenga soko na pia amegawa viwanja. Amekula vya kutosha kwenye hiyo Idara amekuwa nayo, kama ni serikali ya matajiri hata yeye…

Deputy Speaker: Order! Hon. Mutahi. What is it Hon. Stephen Nderitu?

Hon. Stephen Nderitu: Asante sana, Mheshimiwa Spika. Mimi ningetaka Mheshimiwa aweze kunifahamisha na pia kuweka mambo kinagaubaga, wakati anasema mimi niligawa ilhali mimi mwenyewe sio *Surveyor*. Mimi siyo Mwanakandarasi pia, kwa hivyo ningeomba atufafanulie kama yuko na shida ya fikira na hawa watu ambao ni wa Chama cha Jubilee.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Deputy Speaker: Hon. Nderitu, you have to address any Member in this House as a Honourable Member, not *"Huyu"* in quotes. He is an Honourable Member in this House and please accord him his title the way it is supposed to be.

Hon. Stephen Nderitu: Naomba msamaha na pia kutoa hayo matamshi. Nimeona kama Mjumbe Mutahi anatoka kwa mjadala. Wakati anasema hapa mimi niligawa, hiyo nafikiri anaenda kinyume kwa maana hakuna Mjumbe yeyote anaweza gawa. Hivyo ni vile serikali ambayo yeye ni Naibu wa Kiongozi wa Wengi na pia yuko katika Chama ya Jubilee na sisi ambao tuliona mambo yaliharibika tulihama kitambo akabaki peke yake. Hii ni Serikali yao, sisi tuliachana kitambo. Asante.

Hon. Mutahi Muritu: Kweli Mheshimiwa Spika, Sheria ni msumeno hukata mbele na nyuma. Ni vizuri saa zingine tuwe tunamuogopa mungu usije ukakata ule mkono unaokupa chakula. Tukiangalia Mswada tunajadili hapa sasa hivi, ni ripoti ya robo mwaka ya Wizara ya Miundo Mbinu katika Kaunti hii.

Nafikiri kwa sababu anaitetea sana, yeye ni Mwanachama huko na nikiangalia katika ripoti hapa na pia katika ukurasa wa kwanza, yeye yuko pale kama Naibu Mwenyekiti. Sasa amesema alivunja ndoa na ilhali yeye tunapojadili hapa na mimi na serikali yangu ya Jubilee na niliyobaki nikisoma vizuri, yeye ni Naibu wa Mwenyekiti.

Siwezi mwelewa lakini cha muhimu ni kwamba tuwache malumbano. Unajua hawa watu kuna vyama vingine ambazo zilikuwa zimesema zimekwea mlima kumbe walikuwa wanateremka mlima. Mimi niwahakikishie sisi hatuna chaka. Umoja wa Azimio unashinda kwa kishindo katika nchi hii na tutakuwa na Rais ambaye ni mpiganiaji katika nchi hii, nimjibu hiyo.

Nimweleze katika *Leasing program* tusije tukaimeza kazi iliyofanyika na tukijua fika kwamba kuna jambo limefanyika. Kama ni maswala ya malipo ambayo ni miaka iliyoko huko nyuma, hilo tukubaliane kabisa ni kwamba hao ni wawekezaji waliotoka Laikipia. Hao mafao yao tuhakikishe tukiwa kwenye hii Bunge.

Kama kuna hatua tunaweza chukua sasa hivi, tuweze kuchukua kama ni hiyo bajeti ingine inayokuja. Kama ni kusimamisha, tusimamishe na tuhakikishe kwamba tumekuja hapa tumepitisha bajeti ya ziada kwenye miaka matatu iliyopita. Tumekuwa tukiweka zaidi ya milioni mia saba ya kulipa madeni ya hawa watu.

Tunapopokea ripoti kama hii, tujue kwamba wawekezaji kwenye miaka baada ya kuingia kwenye *Leasing program* na *Rentco East Africa* ambaye ni mwekezaji aliyetoka na alipokuja amesaidia. Nikiangalia Mwenyekiti wake sasa hivi bado anaendelea kufanya kazi. Yeye mwenyewe kutoka huko, bado kazi inaendelea vizuri. Sema tu hakukosi changamoto na si eti kwamba natetea upande huo, ni kwa sababu mimi nimekuwa Mjumbe katika Bunge hili.

Jambo lolote ambalo lilichukuliwa hapa ama uamuzi wowote na wewe Mheshimiwa Spika unaelewa vizuri sana. Kama ni maamuzi yaliyochukuliwa kwenye hili Bunge, tulichukua sisi kama Wajumbe. Tusije tukajielekeza katika milengo yetu ya kisiasa kwa sasa hivi kwa sababu ndiyo ni kawaida na ndiyo sababu tuko hapa kwa siasa. Tusije tukazitetea, tutakawa na ushabiki wa kutetea vyama vyetu na ilhali kuna mahali tulikotokea.

Mimi ripoti kama hii napongeza kamati kwa kuona kwamba lakini swali la kujiuliza. Yeye amekuwa mwenyekiti katika kamati ya Uhasibu na Fedha za serikali katika nchi hii, kwa hiyo miaka tano baada ya kupata uteuzi ndiyo amejua kuwa kulikuwa na matatizo? Kwa nini hawakuwasilisha hizo ripoti ndani ya hii Bunge. Tujue kuna watu hawajalipwa, ni kiasi gani za fedha hazijalipwa.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Sasa hivi yeye ni Mwenyekiti wa Bajeti katika hii Bunge. Ukiwaangalia na ni kweli hiyo Chama ni kama siwezi elewa hawa walioteuliwa kwa sababu kidogo napata shaka naona kama ni walanguzi, wamekuja kuteka nyara wananchi wa Laikipia. Yeye ni Mwenyekiti katika Bajeti na pia mwanakamati katika Idara ya Miundombinu.

Sasa mimi kidogo ndiyo na kama mnaichambulia na zingine tuko na shida ya fikira huko tulikotokea kwa sababu sisi ni watu wa *Jubilee* vile anavyoelezea lakini naona. Sawa endeleeni hivyo lakini siku zenu zinakuja; tutakutana kwenye hii Bunge na mtashangaa kwa sababu haya majibu na hii leo iwekwe kwenye kumbukumbu.

Nitamuuliza mwenyekiti yuko pale na pia Naibu wake, hao ni wanachama wa hiyo chama inaleta sindano huwa tunapata tukielekea huko Afrika Mashariki. (*Yellow Fever*) Hiyo kadi ukipata ni kwamba uko na huo ugonjwa, sijui kama ni kisurua ama dui ama ni njia gani. Hao watu mimi saa zingine siwaelewi ama ni huu ugonjwa wamegonjeka…..

Deputy Speaker: Order! Hon. Mutahi. What is it Hon. Jacob?

Hon. Jacob Endom: Mheshimiwa Spika, unajua nimeshangaa kama ni mjadala tuko ama ni kushambuliana. Ninapoana rafiki yangu hata nikisimama ananishambulia, nashangaa kama amechemka ama ni shinikizo amewekwa kwenye kijiji anakuja kuchemukia wengine hapa. Hapa tumekuja mjadala ambao uko katika hii Bunge.

Mambo ya siasa hatukuwa tunaleta katika Bunge. Ukiwa Spika hapo, lazima uone vitu zingine. Usikubalie vitu zingine uongelewe katika hii Bunge. Ukiona mwenzangu amepata shinikizo hata anaweza piga mwingine kofi. Ananilumba na maneno hata wakati sijapata nafasi ya kuongea na yeye. Ni vyema ajue mimi sina ugonjwa, mimi niko sawa na sina shida. Haja yangu ni kujadili mjadala ambao uko katika hili Bunge. Twendeni kwa mjadala, wacha matusi, tukitoka huko nje tutapambana. Unatafuta kura huko na mimi natafuta huko. Sioni ni nini tunakosana na pia sielewi mbona unanitukana mwenzangu.

Deputy Speaker: Thank you, Hon. Jacob. For those words. Indeed you are one of the Eldest in this House and thank you for that guidance. Hon. Members it is true we should stick to the topic of the day and the main debate. Let us stop other things. They will come at the right time at the right place. You may continue Hon. Muritu.

Hon. Mutahi Muritu: Mheshimiwa Spika, nilikuwa nasema ya kwamba hii ripoti inatusaidia na kutupatia mwongozo wa ile bajeti ambayo tunaelekea, ambayo ni ya mwisho wa mwaka na ndipo muhula wetu unaishia na tunafaa kuangalia. Nawahisi Wajumbe wenzangu ya kwamba tusije tukapiga vijembe na sisi ndio tulipitisha. Tatizo kubwa na ile ambayo natetea ni kwamba wale ambao hawajalipwa mafao yao waweze kulipwa. Wale wakubwa kama Mwenyekiti wa Bajeti, naona akitoka mara tu anaposikia bajeti ikitajwa na kujifanya ya kwamba anaenda msalani. Sio msalani ila ni kukwepa ili asisikie kinachoendelea.

Bajeti ya ziada haijamaliza miezi miwili hapa kabla haijapitishwa. Ni kwa nini hawakuweka hizi fedha kwenye hiyo bajeti kama wana haja sana na Wanalaikipia? Hata sisi tunawajali sana wana Laikipia. Mimi Bwana Spika ni kukushukuru wewe na kamati na ninaweza kusikiliza huo mswada na majadiliano watakavyojadiliana lakini kama hao ndio walitayarisha hii ripoti, wanafaa kuitetea kwa sababu ukiangalia kwenye kanuni zetu, hauwezi kuleta ripoti bila kuitetea. Nyinyi ndio mmekuja kuwasilisha lakini tusije kusema ya kwamba hakuna kitu ambacho kimefanyika. Mgala muue na haki umpe. Kazi imefanyika na sidhani ya kwamba kuna mahali ambapo kazi haijafanyika, labda huko Sosian na Rumuruti kwa sababu huko ni mbali sana. Asante, Mheshimiwa Spika.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. Jacob Endom: Asante sana, Bwana Spika. Unajua mwenzangu huko anatetea kwa sababu anajua ya kwamba hayuko kwa huo mlango na hata mwingine akiumia yeye hana haja. Nasimama kuunga hii ripoti mkono. Mwenye kuleta hii ripoti amefanya kazi ya maana kwa sababu ameleta ukweli hapa. Mimi naona ya kwamba mwenzangu hataki mwingine aongee ukweli hapa. Wakati mwingine ukiona mwenzako amenyolewa, hata wewe itafika siku na utanyolewa. Usijione ya kwamba wewe ni mkubwa na hujui ya kwamba hata kesho mwingine anaweza kuwa Gavana. Kwa hivyo nasema ya kwamba hii ripoti ambayo imeletwa kwa hili Bunge ni ukweli mtupu.

Bwana Spika, ukienda kama wadi yangu utashangaa. Ile vita ambayo mwenzangu ameanzisha, ni ile ambayo babake ameanzisha kwa sababu hata babake anatutandika namna hiyo. Ukienda kwangu hakuna hata kazi yoyote ambayo inafanyika. Unaona ya kwamba ameanza kutoka maji. Unaweza kusema ya kwamba kazi imefanyika kwako…

Deputy Speaker: What is it Hon. Muritu?

Hon. Mutahi Muritu: Mheshimiwa Spika, naomba unilinde kwa sababu nimesikia Mheshimiwa kutoka Sosian akitaja babangu. Sasa ningetaka anielezee babangu ni yupi kwa sababu babangu ni marehemu. Sasa sijui kama atafufuka na kuja kupiga kura kama vile wanavyosema kuhusu kura milioni mia moja ya wafu. Hebu atoe ufafanuzi zaidi.

Hon. Jacob Endom: Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa na babangu hapo nje na akaniambia nifuate baba yake. Sasa ndio maana nasema ya kwamba ni babake kwa sababu ameniambia ya kwamba babake atashinda na kwa hivyo nimfuate. Sasa nitamjibu namna gani na yeye mwenyewe ndiye tuliongea naye na kukubaliana? Kwa hivyo mimi nakubaliana na mwenye ameleta hii ripoti katika hili Bunge ya kwamba kuna watu ambao wameadhirika.

Ukienda Sosian, hakuna zile barabara zote ambazo zimeongelewa katika bajeti. Naweza kuambia hii kamati iende Sosian iangalie ile kazi ambayo imefanyika huko ambayo imewekwa katika hiyo bajeti. Waende waangalie kama hiyo kazi imefanyika kisha kuleta hiyo ripoti katika hili Bunge. Nataka kuambia mwenzangu awache kupinga ripoti kwa sababu kwake kazi imefanyika lakini kwa wengine bado kazi haijafanyika.

Tukiwa hapa sisi wote ni kitu kimoja lakini kumetokea mwingine na kusema ya kwamba huyu ni wa chama hiki na mwingine ni wa chama kile. Mimi Jacob siko hivyo, bali niko hapa kutetea watu wangu katika hili Bunge. Sitaki kujua maneno ya vyama lakini kwa sababu umeanza kutufunza, tutafuata yale maneno ambayo umetufunza. Unajua ukifunza mtoto kwenda shule, ataenda na kwa sababu nimesikia mwenzangu ndiye ameanza kuongea hayo maneno…

Deputy Speaker: What is it Hon. Muritu?

Hon. Mutahi Muritu: Mheshimiwa Spika, Nataka Mheshimiwa kutoka Sosian aelezee…

Deputy Speaker: Order Hon. Jacob!

Hon. Mutahi Muritu: Nataka ufafanuzi kwa sababu anasema ya kwamba kuna wadi zingine ambazo zimefanyika nikijua ya kwamba mpango wote umekuwa mpango wa kimkakati hapa. Sasa nashangaa, ni chama kipi? Yeye kwanza ni Kiongozi wa Walio Wachache kwenye hili Bunge na hapa kuna vyama viwili ambavyo ni Jubilee na yake ya PNU. Sasa sijui yeye yuko upande upi juu ameongea vyama. Sasa ananichanganya.

Hon. Jacob Endom: Nimesema ya kwamba ni wewe ndiye umeongelea maneno ya vyama…

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Deputy Speaker: Order! Hon. Jacob and Hon. Muritu! Hon. Muritu, actually you are the one who stated that the works in the other wards have been done and what you are not sure of and suspect have not been done, is only Sosian and Rumuruti. You said that in your earlier conversation. So, you really need to be careful in what you say in this House because it is already on record.

Hon. Mutahi Muritu: Mheshimiwa Spika, sasa hivi tinga ziko Rumuruti na Sosian. Akiri hapa sasa hivi. Zaidi ya miezi miwili tinga ziko huko na sasa naamini ya kwamba kule kazi haikuwa imefanyika ni Sosian na Rumuruti na sasa hizo tinga ziko huko.

Hon. Jacob Endom: Bwana Spika, hapa kuna watu ambao ni mawaziri na hujua mahali kila kitu kipo. Niko na uhakika kabisa kwa sababu niko hapa na pia mwenyekiti yuko. Ningetaka mtoke hapo nje mpige simu mjue kama tinga ziko Sosian kwa sababu huwa mnadanganya kila siku mkisema ya kwamba tinga ziko Sosian. Unajua ni vibaya kudanganya kile kitu ambacho haukielewi mbele wala nyuma. Hakuna tinga ambazo ziko Sosian na ninakiri hivyo.

Ukiangalia hata hii simu yangu, nimejaribu kupiga simu na hakuna mtu hata mmoja ambaye anashika simu zangu kwa sababu nilikuwa nahitaji tinga huko. Kwa hivyo Mheshimiwa ukiongea na hao wakubwa wako, kuwa unaelewa mambo kabisa kwa sababu huwa anadanganywa kwa sababu uliwekwa kwa mfuko na sasa unaletea wengine. Ni lazima ujiheshimu ukiongea hapa kwa sababu ukiongea hivyo nasikia uchungu sana. Kwangu hakujafanywa kazi na unaendelea kusema ya kwamba kumefanywa. Bado ulisimama hapa na kusema ya kwamba Rumuruti na Sosian bado kazi haijafanyika. Sasa tena umesimama na kusema ya kwamba tinga ziko Sosian na Rumuruti.

Mimi siwezi jua kama tinga ziko Rumuruti kwa sababu nasema mambo ya Sosian. Sosian hakuna tinga ambazo zinafanya kazi. Watu wamelalamika na hata walikuwa waandamane kawa sababu wameona ya kwamba hakuna kazi ambayo inafanyika huko. Nilielewa ya kwamba ni mimi ndiye nachapwa kisiasa na nafikiri wewe ni mmoja wa wale ambao wanachangia na ndio maana unasema ya kwamba tinga ziko Sosian.

Mheshimiwa Spika, hayo yote hatujali kwa sababu hii dunia ni mzunguko. Unafikiria ya kwamba unachapa Jacob lakini Mungu naye anafungua njia nyingine ya Jacob ya kupitia. Kwa hivyo mimi naunga mkono hii ripoti kwa sababu ni haki kabisa kuwasilishwa katika hili Bunge kwa sababu kuna watu ambao wametengwa katika hii Kaunti. Hii Kaunti kuna watu ambao wanafanyiwa kazi zaidi ya mara nne ndio wapate kufuata nyuma na kuwatetea. Sio matusi ila ni haki katika hili Bunge.

Bwana Spika, ambia huyu Mheshimiwa ya kwamba sisi huwa tunanyamaza wakati anapoongea na kwa hivyo anafaa kunyamaza tunapoongea, lakini akirudi huko Tigithi anaruhusiwa kupiga kelele hadharani. Hapa ni mahali pa sheria na ni lazima akubaliane na sheria za hili Bunge. Kwa hivyo naunga mkono na kwa sababu ameanza kutoroka, wacha nikae chini.

Deputy Speaker: May I call upon the mover to give a reply?

Hon. Daniel Mugweru: Thank you, Hon. Speaker. I wish to thank the Hon. Members who have participated and also supported the report. I believe that it will really help us in making decisions especially when we will be preparing the budget. As much as you see confrontation in the House, when stress is prolonged, it turns into depression. When you see somebody pointing another with arrogance, it tells that stress has turned into depression and

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

that tells you that we need somebody who can do counselling before our minds are messed up. Thank you.

Deputy Speaker: Hon. Members, I defer the putting of the question until tomorrow morning. This will be the first business which we will conduct as soon as we get into the chambers.

(Motion deferred)

ADJOURNMENT

Deputy speaker: The sittings of this House stands adjourned until tomorrow Wednesday, 8th June, 2022 at 9.00 a.m.

The House rose at 3.08 p.m.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*